

HOTUBA YA MSTAHIKI MEYA WA JIJI LA DAR ES SALAAM, MHE. ISAYA
MWITA CHARLES, WAKATI AKIMKARIBISHA WAZIRI WA NCHI OFISI YA
RAIS TAMISEMI. MHE. SULEIMANI JAFFO(MB) KATIKA UZINDUZI WA KAZI
ZA KUKUZA UTALII KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM

17 MACHI, 2018

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani
Jaffo(Mb),**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Paul Makonda,

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mheshimiwa Sophia Mjema,

Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita Charles,

Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam,

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bi. Theresia Mmbando,

**Wakurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke, Ubungo,
Kigamboni,**

Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Jiji,

Wageni waalikwa,

Ndugu wananchi,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana,

Ninaomba kuchukua fursa hii, awali ya yote, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusimama nasi wakati wote katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam. Mafanikio tuliyonayo katika Halmashauri ya Jiji yanatokana na Baraka zake Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hiyo ndiyo maana tupo hapa leo kushuhudia mojawapo ya sehemu ya mafanikio yetu katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo na tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Ninakushukuru sasa kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi. Tumefarijika sana. Halmashauri ya Jiji kwa muda mrefu imekuwa ikifanya maandalizi ya kuibua na kuviainisha vivutio vya utalii vya Dar es Salaam. Tumebaini kwamba Dar es Salaam kuna vivutio vingi vya utalii vinavyohusu historia ya nchi hii, mila, desturi na utamaduni, majengo ya kihistoria, siasa, uchumi na mambo ya jamii. Lengo letu ni kuvitangaza vivutio hivyo ili kukuza utalii katika Jiji la Dar es Salaam.

Vivutio vya utalii tulivyonavyo ni hadhina kubwa ya kuongeza mapato ya Jiji, ajira kwa wananchi wetu pamoja na uhifadhi wa mazingira. Baraza la Madiwani la Jiji liliazimia kwamba tuelekeze nguvu zetu katika sekta hii kwa kukuza utalii wa ndani, ambao kwa kiasi kikubwa una mwamko mdogo wa ushiriki kutokana na kukosekana kwa ushawishi wa kuwavutia wananchi na kuwawezesha kutambua wajibu wao wa kushiriki katika kukuza utalii ndani

na nje ya nchi. Kwa kutoshiriki kwao, Jiji kwa namna moja au nyingine imekuwa ikikosa mapato ya ndani.

Kwa upande wa watalii kutoka nje ya nchi, changamoto zake ni nyingi. Kila siku tunawaona wakipita kuelekea sehemu nyingine za nchi wakituacha na Dar es Salaam yetu. Tumejiuliza sana. Tukapata majibu. Tumeamua kuwekeza katika Sekta ya Utalii na tumeanza sasa, ingawa tumechelewa. Ninapenda kukuhakikishia kwamba tutafanikiwa kwa kiasi kikubwa katika mipango yetu ya kukuza utalii katika Jiji hili.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Tumefanikiwa katika eneo la uhifadhi wa majengo kwa kushirikiana na wadau kwa kutambua kwamba hii ni sehemu mojawapo ya vivutio vikubwa vya utalii. Bado tutaendelea na kazi hiyo hadi tutakapofanikiwa kufikia malengo yetu kwa kuwa ukiachia Jengo la Old Boma bado tunayo majengo mengine mengi ikiwemo jengo letu la City Hall. Ununuzi wa mabasi ya kuhudumia watalii ni hatua kubwa ya mafanikio kwa Jiji. Tunapenda Jiji likiwa pia na maboti yanayotoa huduma za usafiri wa majini kwa watalii na katika hili tutashirikiana sana na sekta binafsi.

Sekta binafsi ni muhimu sana katika maendeleo ya sekta ya utalii nchini na kwa kulitambua hilo tumeamua kutoa mafunzo ya namna ya kuhudumia watalii kwa wenzetu madereva wa teksi na mama lishe. Kwa kulitambua hilo, tumejipanga kuwapatia mafunzo baadhi ya wadau kama vile mateksi

dereva na mama lishe. Tutaendelea kutoa mafunzo hayo kadri tutakavyopata fedha.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuutangaza utalii. Suala hili ni mtambuka na linahitaji juhudi kubwa kutoka katika Wizara na sekta mbalimbali za Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kutoka katika sekta binafsi. Tunakuomba ulichukue hilo ili tuunganishe nguvu zetu katika kuvitangaza vivutio vya utalii vya Dar es Salaam na kuiwezesha Halmashauri ya Jiji kutimiza malengo yake kwa maslahi ya watanzania.

Pamoja na hilo ni lazima tutengeneze mazingira mazuri ya kuwafanya watalii wabaki Dar es Salaam. Tumeshalianza hilo kwa kutengeneza na kuboresha bustani zetu, sehemu za kupumzikia, sehemu za kucheza ngoma za jadi na kuboresha huduma zetu kwa watalii.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Nilisema kwamba nimefarijika sana kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi. Yapo mengi tutayafanya kuunga mkono juhudi za Serikali za kukuza utalii nchini. Tumeamua kuanza kwa vitendo. Tunakuahidi tena kwamba tutaendelea na juhudi zetu za kufanikisha kazi hiyo. Asante sana na ninakuomba sasa uongee na wananchi kupitia hadhara hii.